VERMONT
DEPARTMENT OF LABOR

# MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA: MAMBO YA UJUMLA KUHUSU BIMA YA UKOSEFU WA AJIRA

**Kuweka Dai la Mwanzo:** Piga 1-877-214-3330 au 1-888-807-7072, au weka maombi mtandaoni kwenye www.labor.vermont.gov

**Kufungua Dai za Wiki:** Piga: 1-800-983-2300 (Lain ya Kiautomatiki (masaa 24 Jumapili, 5asubuhi - 4:30jioni Jumatatu-Ijumaa), mtandaoni: www.labor.vermont.gov

**Je, unatafuta taarifa zaidi kuhusu Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira? Tembelea https://labor.vermont.gov/PUA**

---

## SIFA

**Je, nina sifa za kupata mafao ya ukosefu wa ajira?**
Matakwa ya sifa za mafao ya ukosefu wa ajira yamepanuliwa kutokana na COVID-19 ili kujumuisha maeneo yafuatayo:

- *Unaweza kuwa na sifa ikiwa uliachishwa kazi kutokana na:*
    - Mwajiri wako kusimamisha uendeshaji kutokana na sababu inayohusiana na COVID-19
    - Tokeo la moja kwa moja la oda iliyotolewa na gavana ama rais
    - Waajiriwa waliojitenga/kujiweka karantini kutokana na COVID-19
- *Unaweza kuwa na sifa ikiwa uliacha kazi kutokana na:*
    - Kuwa mgonjwa ama kujitenga kutokana na COVID-19

    - Kuwa na hatari ya kupata ugonjwa kwenye sehemu yako ya kazi
    - Kumlea mwana familia anayeumwa ama aliyejitenga kutokana na COVID-19
    - Kumlea mwana familia ambaye amekuwa hatarini kupata ugonjwa eneo lake la kazi
    - Kuwa na haja ya kumlea mtoto ambaye shule au kituo chake cha malezi ya watoto kimefungwa

**Itakuwaje ikiwa nimeambiwa na mtaalamu wa matibabu au afisa wa afya jamii nijitenge kutokana na COVID-19, licha ya kuwa siumwi?**
Unaweza kuwa na sifa ya kupata mafao ya ukosefu wa ajira ikiwa umefikia vigezo vifuatavyo:

- Unafuata muongozo wa mtaalamu wa matibabu ya afya au afisa wa afya jamii wa kujitenga au kujiweka karantini kutokana na kuwa kwenye hatari ya kupata COVID-19
- Haupokei malipo ya likizo ya ugonjwa au likizo nyingine zozote kutoka kwa mwajiri wako

**Itakuwaje ikiwa mwajiri wangu amesimamisha uendeshaji, kama hatua ya tahadhari au kwasababu ya mwajiriwa kuumwa, na waajiriwa wengine kuombwa kujitenga ama kujiweka karantini kutokana na COVID-19? Nitakuwa na sifa ya kupata mafao ya ukosefu wa ajira?**
Ikiwa haupokei fidia kutoka kwa mwajiri wako, kama malipo ya likizo ya ugonjwa au likizo ya malipo, unaweza kuwa na sifa ya kupata mafao ya ukosefu wa ajira katika kipindi hichi.

**Ikitokea nimeumwa sana na nimelazimika kuacha kazi kutokana na COVID-19, je nitastahili kupata mafao ya ukosefu wa ajira?**
Ndio. Matakwa ya sifa za mafao ya ukosefu wa ajira yamepanuliwa kujumuisha watu wanaoumwa ama waliojitenga kutokana na COVID-19.

**Itakuwaje ikiwa nitahitaji kuacha kazi yangu ili kulea mwana familia kutokana na COVID-19?**
Ikiwa utaacha kazi ili kumlea mwana familia, utakuwa na uwezekano wa kuwa na sifa ya kupata mafao ya ukosefu wa ajira.

**Mwajiri wangu amefunga uendeshaji kwasababu ya COVID-19, je nina sifa?**
Ikiwa mwajiri wako amefunga kwasababu ya COVID-19, unaweza kuwa na sifa ya kupata Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira (PUA) au ukosefu wa ajira wa mara kwa mara.

**Mwajiri wangu amepunguza masaa yangu ya kazi kwasababu ya COVID-19, je nina sifa?**
Ikiwa mwajiri wako amepunguza masaa yako ya kazi kwasababu ya COVID-19, unaweza kuwa na sifa ya kupata mafao ya ukosefu wa ajira.

**Je, itakuwaje ikiwa eneo langu la kazi limefungwa lakini ninafanya kazi nikiwa nyumbani, nitakuwa na sifa?**
Ikiwa eneo lako la kazi limefungwa kwa umma, hata hivyo unafanya kazi ukiwa mbali na kazini, bila kuwa na punguzo la mshahara, hautakuwa na sifa ya kukosa ajira.

**Mwajiri wangu alitaka nirudi kazini, lakini sikujihisi salama kurudi. Je, nitaweza kutokurudi kazini na bado nikaweka madai ya ukosefu wa ajira?**
Kushindwa kukubali kazi wakati ukiwa na uwezo pamoja na uwepo wa kufanya hivyo, kutakuondoa katika sifa ya mafao ya ukosefu wa ajira.

# MASWALI YANAYOHUSIANA NA MADAI

**Nimepokea “uamuzi wa kifedha,” hii ni nini na ina maana gani?**
Uamuzi wa Kifedha wako unahesabiwa kwa msingi wa mishahara ya ndani ya robo awamu 4 zilizopita. Uamuzi wa fedha unayopokea ni kiasi cha mafao ya nchi na hakiakisi nyongeza ya $600 za mafao ya serikali yaliyoongezwa kutoka kwenye sheria ya CARES. $600 zitaonekana kwenye fedha zako za kieletroniki ama cheki ya karatasi.

**Je, nifungue dai jipya ikiwa nilifungua dai la ukosefu wa ajira mwaka uliopita na nikarudi kazini?**
Ikiwa una dai lililofunguliwa ndani ya miezi 12 iliyopita, hautohitaji kurudia kujisajili kwenye ukosefu wa ajira. Unaweza kulifungua dai lako kwa kurudi na kuingia kwenye tovuti ya mdai ya mtandaoni ama kwa kupiga simu kwenye lain ya kiautomatiki ya madai ya wiki. 1-800-983-2300 (masaa ya lain ya kiautomatiki: masaa 24 Jumapili, 5asubuhi-4:30jioni Jumatatu-Ijumaa)

**Itakuwaje ikiwa dai langu limekwisha muda wake?**
Ikiwa dai lako limekwisha muda wake, utakuwa na sifa ya kupata mafao yaliyoongezeka ambayo hujumuisha wiki 13 za nyongeza za mafao. Programu hii ya mafao yaliyoongezwa iko katika uchukuliwaji hatua. Idara itatangaza pale programu itakapokuwa hewani.

**Nilisahau kuweka dai langu la wiki, wiki iliyopita. Nifanyeje?**
Ikiwa ulisahau kuweka dai la wiki kwenye wiki iliyopita, unaweza kupiga simu kwenye lain ya kiautomatiki ya dai za wiki katika 1-800-983-2300 ama kuingia kwenye tovuti ya mdai ya mtandaoni na kuweka dai la wiki iliyopita. Unaweza tu kuweka dai la wiki moja iliyopita katika siku. Utapokea ujumbe kwenye ukurasa wa uthibitisho utakaokujulisha lini utaweza kuingia tena kwenye tovuti ya mdai na kuweka dai jingine linalokosekana. Ukishamaliza, utahitaji kuendelea kuweka dai za wiki kila wiki kwanzia Jumapili mpaka Ijumaa saa 4:00 jioni.

**Dai langu linasema kuwa linaamuliwa. Hii inamaana gani?**

Madai yaliyowekwa kwenye uamuzi huwa yanahitaji kupitiwa zaidi na Idara ili kuhakiki ustahiki. Baadhi ya yaliyopo zaidi ni pamoja na, kushindwa kuripoti mishahara kwa siku moja au mbili za kazi. (Mfano. Ikiwa ulifanya kazi Jumatatu – Jumatano na ukasimamishwa kazi Alhamisi, utapaswa kuripoti mishahara ya Jumatatu – Jumatano). Idara itakutaarifu pale uamuzi utakapokamilika.

## MASWALI YANAYOHUSU MALIPO

**Kwanini sijapokea mafao kamili ya $600?**

Utakapomaliza maombi yako ya kwanza, ikiwa ulichagua kodi zako zizuiliwe kwenye kiasi chako cha mafao ya wiki, kodi zitazuiliwa pia kwenye mafao yako ya serikali $600. Mafao yatahusika katika kodi za serikali na nchi.

**Nitapata mafao kwa muda wa kipindi gani?**

Unaweza kupokea mafao ya bima ya ukosefu wa ajira kwa wiki 26 na nyongeza ya mafao kwa wiki 13.

**Nitalipwa kipindi gani?**

Ikiwa utawasilisha dai zako za wiki kwa mfululizo na hautakuwa na shida zozote kwenye madai yako, unaweza kutarajia kulipwa kwa msingi wa kila wiki.

**Niliwasilisha maombi yangu ya ukosefu wa ajira lakini sijapokea pesa yoyote. Kwanini?**

Baada ya kuwasilisha ombi lako la kwanza, utabidi kuendelea kuwasilisha madai ya kila wiki utakayokuwa huna kazi. Kila dai la wiki linahakiki kuwa hukuwa na ajira katika wiki iliyopita. Kama hautoweka madai ya wiki, mfumo utadhania kuwa umerudi kazini na utaacha kutoa mafao.

**Niliwasilisha maombi yangu ya ukosefu wa ajira, nimekuwa nikiwasilisha madai yangu ya wiki, hata hivyo sijapokea pesa yoyote. Kwanini imekuwa hivyo?**

Ikiwa bado haujapokea mafao yoyote ya ukosefu wa ajira, ikiwa ni pamoja na cheki ya malipo ya awali ya $1200, dai lako litakuwa na shida ambayo inahitaji Idara kufanya utafiti zaidi ili kuhakiki ustahiki. Hii inaweza kutokana na haja ya Idara kukusanya taarifa kutoka kwenye nchi nyingine, masuala ya mapato, na vinginevyo. Idara itakutaarifu

pindi mchakato wa uamuzi utakapokamilika.

## MASWALI MENGINE KUHUSU BIMA YA UKOSEFU WA AJIRA

**Ninarudi kazini. Je, nitapaswa kufanya chochote kuwataarifu Idara ya Wafanyakazi?**
Ikiwa unarudi kazini, hautohitaji kuwataarifu Idara wakati huu. Utapaswa tu kuacha kuweka madai yako ya wiki. Ikiwa utaweka madai ya wiki huku ukiwa umeajiriwa kikamilifu, hilo litakuwa tendo la udanganyifu na utakoseshwa mafao yako. Kama unafanya kazi ambayo unaweka madai ya mafao ya UI, utapaswa kuripoti masaa ambayo umefanya kazi na mshahara uliopata.

**Dai langu liko katika uamuzi kwa wiki kadhaa sasa. Je, kuna mpango wowote wa nyakati unaonyesha lini nitapokea maamuzi?**
Ikiwa dai lako liko katika kufanyiwa maamuzi, litaamuliwa kwa mpangilio wa jinsi lilivyopokelewa.

**Ninatengenezaje upya neno langu la siri (PIN)?**
Ikiwa unahitaji kutengeneza upya neno lako la siri (PIN), unaweza kupiga simu kwenye lain yetu ya ziada kwenye 888-807-7072.

**Teyari nilikuwa sina ajira kabla ya COVID-19, bado nitahitaji kutafuta kazi?**
Hapana. Mahitaji yote ya tafuti za kazi yamesimamishwa kutokana na COVID-19. Idara itawataarifu wadai pindi mahitaji ya tafuti za kazi yatakaporejea.

**Tarehe yangu ya kurudi kazini imekwishapita. Sijajua lini nitarudi kazini, namna gani ninaweza kurekebisha hilo?**
Kwa sasa, hauhitaji kurekebisha tarehe yako ya kurudi kazini. Idara itatangaza mabadiliko yoyote ya kwenye mfumo huu.

**Kwanini ninapata 'SSN haijapatikana' wakati nikiweka dai langu la wiki?**
Kuna uwezekano kuwa unapata 'SSN haijapatikana' kutokana na moja ya sababu zifuatazo:

- Dai lako la mwanzo kuwa bado kwenye mchakato. Inaweza kuchukua hadi masaa 72 ya kazi kwanzia muda ulipowasilisha dai lako la mwanzo, hadi dai lako kupakuliwa kwenye mfumo.
- Unajaribu kuweka dai mapema sana ama kwa kuchelewa sana. Dirisha la uwekaji dai za wiki hufunguliwa Jumapili hadi Ijumaa saa 4:00 jioni.
- Dai lako linafanyiwa maamuzi. Ikiwa kuna tatizo kwenye dai lako, litakuwa limekabidhiwa kwa muamuzi. Hautaweza kufungua tovuti ya mdai mtandaoni, mpaka pale dai lako litakapoamuliwa.